SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM)

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024

MEI, 2023

YALIYOMO

A. UTANGULIZI.....1
B. MAJUKUMU YA WIZARA 3
C. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....4
D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....4
E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....6
F.MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/20244 38
G.MAENEO YA VIPAOMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 39
H. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.....41
I. SHUKRANI 52
J. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2023/2024 53
VIAMBATANISHO 54
KIAMBATISHO NAMBA 1 A.....55
KIAMBATISHO NAMBA 1B.....58
MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023.....58
KIAMBATISHO NAMBA 1C.....58
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA 58
KIAMBATISHO NAMBA 1D.....58
FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO.....60
KIAMBATISHO NAMBA 1E.....61
FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO 61
KIAMBATISHO NAMBA 1F 63

BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNINA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 64
KIAMBATISHO NAMBA 1G..... 66
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA KILA PROGRAMU NDOGO 66
KIAMBATISHI NAMBA 1H 69
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 69
KIAMBATANISHO NO 1I 69
MAPATO YATAKAYO KUSANYWA NA YANAYOTUMIWA NATAASISI HUSIKA 69
KIAMBATANISHO NO. 2A 70
ORODHA YA VIJANA WALIOPATIWA WA MAFUNZO MBALI MBALI 70
KIAMBATANISHO NO 2B 71
MCHANGANUO WA VIKUNDI UNGUJA..... 71
MCHANGANUO WA VIKUNDI PEMBA 71
KIAMBATANISHO NAMBARI 3A 73
VYAMA/VILABU VYA MICHEZO MBALI MBALI VILIVYOSHIRIKI MASHINDANO YA KIMATAIFA 2022/2023 73
KIAMBATANISHO 3B 74
VYAMA/VILABU VYA MICHEZO MBALI MBALI VILIVYOSHIRIKI MASHINDANO YA KITAIFA 2022/2023 . 74

HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema pamoja na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa pumzi ya kusimama mbele ya Baraza lako kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa kiongozi wetu, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo tangu kuanza kwa utawala wa awamu ya nane. Ni heshima kubwa kwangu kufanya kazi chini ya Kiongozi Mkuu wa nchi ambaye ana upeo mkubwa sana, mchapa kazi, mwenye uzalendo wa kweli na ambaye amestaajabisha dunia kwa kutekeleza mambo makubwa ya kimaendeleo kwa kipindi kifupi. Itoshe tu kusema namshukuru sana, naendelea kumuombea afya njema yeye na familia yake ili kazi kubwa aliyoianza ya kuwaletea maendeleo makubwa wananchi wa Zanzibar iweze kukamilika.

3. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais kwa namna walivyojitoa katika kuwahudumia wazanzibari. Nimefurahi kufanya

kazi chini yao na ninawasihi wazanzibari kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaidizi hawa waandamizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni makini na wenye mapenzi ya dhati kwa nchi yao. Tuendelee kwa pamoja kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuwa na afya njema, hekima na busara katika kazi zao za kumsaidia Kiongozi Mkuu wa nchi.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kusimamia muhimili huu wa Baraza la Wawakilishi kwa umahiri mkubwa sana. Aidha, ninakupongeza pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bajeti za Wizara mbali mbali.

5. **Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba pia nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mahiri na Mchapa kazi Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2023/2024. Nakiri kwamba, mimi binafsi na watendaji wa Wizara yangu na Taasisi zake tumejifunza mambo mengi mazuri kutokana na hoja na ushauri wa Kamati hii.

6. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, napenda nitumie fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote wa Serikali ya awamu ya nane kwa kusimamia majukumu ya Wizara zao vizuri na kupelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020 - 2025.

7. **Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti, Makamo Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa ushauri

na maelekezo wanayoyatoa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa ufanisi katika Serikali ya awamu ya nane.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu. Nitaanza kwa kuelezea majukumu ya Wizara, programu za Wizara, mapitio ya utekelezaji wa mipango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, maeneo ya vipaombele pamoja na mikakati mbali mbali ambayo itatekelezwa na Wizara kwa mwaka 2023/2024. Aidha, nitawasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa Programu kuu nne (4) na Programu ndogo nane (8).

9. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hizi umezingatia vipaombele vilivyomo kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2021-2026 na Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

B. MAJUKUMU YA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa majukumu ya kisera na kiutendaji ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ni pamoja na haya yafuatayo:-

    i. Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari (Magazeti, Vituo vya Redio na Televisheni);
    ii. Kusimamia, kuratibu na kudhibiti habari na huduma za utangazaji;
    iii. Kuratibu huduma za uchapaji na kusimamia shughuli za Mpiga chapa Mkuu wa Serikali;
    iv. Kusimamia, kuendeleza na kukuza Lugha ya Kiswahili.
    v. Kusimamia maendeleo na ukuzaji wa sanaa na utamaduni wa mzanzibari;
    vi. Udhibiti wa filamu na tamthilia;
    vii. Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

viii. Kuratibu na kusimamia programu mbali mbali za Maendeleo ya Vijana;

ix. Kusimamia na kukuza sekta ya michezo;

x. Kukuza kampeni ya Zanzibar ya 'Michezo kwa Afya'; na

xi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta husika.

C. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imetekeleza Programu kuu nne (4) na Programu ndogo nane (8) chini ya Fungu J03. Programu kuu ni hizi zifuatazo:

i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji;

ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana;

iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

iv. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilikadiriwa kupata **shilingi 49,081,861,000/-** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza Programu kuu nne. Kati ya fedha hizo **shilingi 16,344,600,000/-** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi**

32,737,261,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za matumizi ya kazi za kawaida, **shilingi 8,385,000,000/-** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 7,959,600,000/-** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilipangiwa kukusanya **shilingi 875,997,000/-** ambayo ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Utekelezaji kifedha kwa mwaka 2022/2023

14. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 12,223,435,806/-** zimepatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 25 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo **shilingi 11,663,435,806/-** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na **shilingi 560,000,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

15. **Mheshimiwa Spika,** aidha, fedha zilizopatikana za matumizi ya kazi za kawaida, **shilingi 9,185,354,935/-** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 79 na **shilingi 2,478,080,871/-** sawa na asilimia 21 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiambatanisho nambari 1A -1D kinahusika.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa makusanyo halisi yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023, ni **shilingi 492,009,117** sawa na asilimia 56 ya makadirio ya mwaka. Kiambatanisho nambari 1B -1D vinahusika.

E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji

17. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 22,980,061,000/-**, kati ya fedha hizo, **shilingi 4,619,200,000/-** ni mishahara, **shilingi 4,023,600,000/-** ni matumizi mengineyo na **shilingi 14,337,261,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

18. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 6,402,326,435/-** zimepatikana sawa na asilimia 28 ya makadirio. Kati ya fedha hizo **shilingi 5,391,027,435/-** ni mishahara sawa na asilimia **84**, **shilingi 1,011,299,000/-** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **16** na hadi kufikia machi hakuna fedha iliyopatikana kupitia Miradi ya Maendeleo.

Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

19. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika Magazeti ya Serikali (SMS) na Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shillingi 19,391,261,000/-**. Kati ya hizo **shilingi 7,054,000,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 12,337,261,000/-** kwa Miradi ya Maendeleo.

20. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya **shilingi 5,127,736,760/-** zilipatikana sawa na asilimia 26. Kati ya fedha hizo, **shilingi 5,127,736,760/-** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kupitia Miradi ya Maendeleo. **(kiambatanisho namba 1A na 1D kinahusika).**

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2022/2023 shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa nazo ni:- kuboresha huduma ya utoaji wa taarifa, picha, makala, filamu na sinema, kuzalisha na kurusha vipindi na matangazo kupitia ZBC TV na Redio, kusambaza maudhui ya utangazaji kupitia ZMUX, kuchapisha magazeti na kuyasambaza, kuwajengea uwezo wafanyakazi wa mashirika na kueka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi.

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kuandika na kusambaza taarifa **508** za kiuchumi, kisiasa na utamaduni zikiwemo ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na viongozi mbali mbali, uzinduzi wa miradi ya maendeleo, mikutano ya waandishi na viongozi wa Serikali. Taarifa hizo zilisambazwa kupitia vituo vya habari vya umma na binafsi. Sambamba na hilo, Wizara imeuza picha za Viongozi Wakuu wa nchi **362** zikiwemo picha **120** za Rais wa Zanzibar, picha **224** za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, picha **4** za Rais Wastaafu na picha **14** za Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mikutano miwili ya kuwajengea uwezo Maafisa Habari na Mawasiliano ambapo Maafisa **65** wa Serikali kutoka Wizara 18 walishiriki. Kupitia mafunzo hayo Maafisa Habari waliweza kujua majukumu yao kama watendaji wa Serikali na Muundo wa Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini. Kadhalika, Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa maafisa habari 27 kutoka Zanzibar katika mafunzo yaliyoandaliwa na Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano Tanzania (TAJCO). Maafisa hao waliweza kujifunza taaluma ya ufanisi wa picha na jinsi ya kuripoti taarifa na kuwa mabalozi wakati wa sensa kwa kuzingatia usalama wa matumizi ya TEHAMA. Pia,

maafisa habari 12 kutoka Zanzibar waliweza kushiriki katika Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari lililoandaliwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Tanzania. Kupitia kongamano hilo maafisa waliweza kujifunza kutoa taarifa kwenye tovuti na mitandao ya kijamii kwa wakati.

24. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar (SMS) linaendelea na kutekeleza jukumu lake la msingi la kuchapisha Gazeti la Zanzibar Leo, Zanzibar Mail, Zanzibar Leo Jumapili, Zaspoti na Gazeti la kila mwezi Zanzibar Leo Wanawake na kuyasambaza katika Mikoa 5 ya Zanzibar na mikoa **25** ya Tanzania Bara. Pia, Shirika limefanikiwa kuongeza idadi ya mawakala kutoka 14 hadi 36 na wauzaji wadogo kutoka **22** hadi **150.** Lengo ni kutoa habari, kuelimisha kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, kutoa burudani na taarifa za kimichezo pamoja na kutangaza sera, mikakati na mipango ya Serikali.

25. **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilipanga kuchapisha nakala **918,000** kwa magazeti yake yote na limefanikiwa kuchapisha nakala **944,000** sawa na asilimia **103** hadi kufikia mwezi Machi 2023. Aidha, Shirika lilipanga kutoa matangazo **2000** na kufanikiwa kutoa matangazo **1,020** sawa na asilimia **51**. Kupungua kwa kiwango cha matangazo kumetokana na uhaba wa fedha kwa taasisi mbali mbali na ushindani mkubwa wa kibiashara katika sekta ya habari. Vile vile, Shirika limeanzisha jarida maalumu linaloitwa Neema Zetu, Fahari Yetu lenye lengo la kuwaeleza wananchi juu ya Neema (Utekelezaji wa Serikali ya awamu ya nane) ambazo Mheshimiwa Rais anaendelea kuwaletea. Jarida hili limesambazwa bure katika Shehia zote za Zanzibar, Taasisi za umma, Asasi za kiraia na binafsi.

26. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanikiwa kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kwenda kidijitali katika utendaji kazi za Shirika ili kuendana na mabailiko ya teknolojia. Kwa sasa, magazeti yanatangazwa kupitia mitandao ya kijamii kama vile **Instagram, Facebook, Twitter, Youtube** na kupitia website ya Shirika ambayo ni ***www.smsz.co.tz*** Pia, magazeti yanauzwa kupitia mfumo wa ***e-paper*** kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake kwa wasomaji popote duniani. Jumla ya nakala 894 zimeuzwa kupitia mfumo wa e-paper yakiwemo magazeti ya Zanzibar leo 867, Zanzibar mail 75 na Zaspoti 51. Napenda kutoa wito kwa watendaji wa Serikali, taasisi za kiraia na wananchi kwa ujumla kuendelea kutuunga mkono kwa kuyasoma magazeti na kutangaza biashara zao kupitia Shirika la Magazeti ya Serikali kwani bei zetu ni nafuu mno.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati, Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) limeweza kuandaa na kurusha hewani vipindi na matangazo kupitia TV na Redio pamoja na mitandao ya kijamii. Jumla ya matangazo **17,614,** vipindi vya nje **1,420** na vipindi vya ndani **11,427** vimerushwa hewani kupitia ZBC TV. Miongoni mwa vipindi hivyo ni Rahatu Zaman, Shani ya Mola, Urithi wetu, Ukweli si uvumi, Dau la Habari, Chowea, Zanzibar Wiki hii, ZBC Dokta, Ajira ni Biashara na Muelekeo wetu. Vipindi vyengine vilivyorushwa hewani ni pamoja na vipindi vya Watoto na Burudani, Michezo na Maigizo, makala na habari kutoka katika channel mbali mbali za nje.

28. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limefanikiwa kurusha hewani vipindi **12,753** kwa upande wa ZBC Redio na **6,324** kwa upande wa Spice FM. Vipindi hivyo ni pamoja na Kurunzi ya ZBC, Asili zetu, Usiku wa zilipendwa, Nuru ya Quran, ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar pamoja na Viongozi

Wakuu wa Serikali, vipindi vya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar na vipindi vya kawaida vikiwemo kutoka jimboni, Mazungumzo ya asubuhi, Mawio, Badilika, Thamani yangu, Afrika yetu, Tungo zetu, Vijana, Utalii wa ndani, Michezo, Sauti yao na Weekend special.

29. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limeweza kurusha matangazo ya moja kwa moja (live) **128**, ikiwemo Maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi, Kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa, Uzinduzi wa Mwenge wa Uhuru Kitaifa na ufunguzi na uwekaji wa mawe ya msingi ya miradi ya maendeleo nchini.

30. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limefanikiwa kuanzisha vipindi vipya vikiwemo kutoka Sokoni, Nijuze na Ijue Afya yako na vipindi ambavyo bado havijarushwa hewani ikiwemo uchumi wa Bluu, Sauti za Watoto na Jukwaa la Vijana.

31. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Redio na kipindi cha maisha na kipindi cha mwega wa maisha kwa upande wa TV. Vile vile, Shirika limefanikiwa kufanya vikao 4 vya Bodi ya Wakurugenzi vilivyojadili ajenda mbali mbali zikiwemo utekelezaji wa shughuli za Shirika, Mpango wa mageuzi ya Shirika, taarifa za fedha za ZBC na Mpango wa manunuzi wa ZBC kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

32. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uunganisha na Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) imeendelea kuimarisha na kusimamia shughuli za uendeshaji wa vituo saba vya urushaji maudhui Unguja na Pemba ili kuhakikisha huduma inapatikana muda wote na kwa utulivu (signal stability). Sambamba na hilo, ZMUX imeandaa Mpango mpya wa Uwekezaji (New Investment Plan), ambapo kupitia mpango huo Kampuni itafanya mabadiliko makubwa yakiwemo mageuzi ya kimfumo na ubora wa

maudhui (contents) yenye kuwavutia watazamaji wengi na yatakayowezesha kuipatia Kampuni faida na kutoa gawio Serikalini. Uwekezaji huo tayari umeshapata baraka za Serikali na unatarajiwa kuanza mapema katika mwaka wa fedha 2023/2024.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya ZMUX imeweza kuziboresha chanali zake za ZMUX TAQWA, ZMUX CINEMA, ZMUX MOVIES na ZMUX SWAHILI kwa kuweka vifaa vipya na kutayarisha vipindi mbali mbali kikiwemo kipindi cha Tambo za Mwambao. Aidha, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi walipata fursa ya kwenda kujifunza namna ya Taasisi za Uunganishaji Maudhui zinavojiendesha na kupata faida. Miongoni mwa Kampuni walizotembelea ni Azam Media na Star Times zilizopo Dar es Salaam. Pia, ZMUX imeandaa mpango maalumu wa kufikisha huduma ya upatikanaji wa habari Tanzania Bara kwa lengo la kuongeza wigo wa kibiashara. Hatua za awali zimekamilika ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kupata ushauri wa kitaalamu na miongozo ya kisheria. Mpango huu unatarajiwa kuanza kazi mwaka 2024 mara tu utakapokamilika mpango wa uwekezaji wa Kampuni.

Mradi wa Uimarishaji Utowaji wa Matangazo ZBC

34. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uimarishaji Utoaji wa Matangazo ZBC unatekelezwa katika Programu ndogo ya Upatikanaji na Utoaji wa Habari. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu ulipangiwa jumla ya **shilingi 12,337,261,000/-** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kurushia matangazo. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, Mradi haukuingiziwa fedha.

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar. kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shillingi 3,626,515,000/-** ambapo **shilingi 1,626,515,000/-** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

36. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Machi, 2023 jumla ya shilingi 1,864,418,755/- zimepatikana sawa na asilimia 51 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. (kiambatanisho namba 1A na 1D vinahusika).

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2022/2023 shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa kudhibiti na kusimamia vituo vya utangazaji kupitia sera na sheria, kuboresha huduma za bohari kwa kuongeza vifaa vya ofisi na kuandikia, kununua mitambo ya kisasa ya uchapaji, kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

38. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kudhibiti, kusimamia na kuwawezesha Waandishi wa Habari waliopo nchini kufanya kazi zao bila ya vikwazo, Wizara imetoa vitambulisho **500** vya Waandishi wa Habari wanaofanya kazi katika vituo vya utangazaji na magazeti mbali mbali hapa nchini. Aidha, vibali **14** vya uchukuaji wa picha za kutengenezea filamu vimetolewa kwa makampuni yanayojishughulisha na uandaaji wa filamu ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa kampuni hizo ni Hans Otto Film GbR kutoka Ujerumani, Hibiscus tours and Safari ya Zanzibar, RED kutoka USA, Burning Bright Production

ya Uingereza na ZDF Germany TV. Pia, Wizara imetoa kibali cha wakala wa Habari kwa mpiga picha Ndugu; Damian Wasiewsiki anayefanyia kazi katika Kampuni ya Zambwas Company Limited iliyopo Jambiani Zanzibar.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba vituo vya utangazaji Zanzibar vinafuata sheria na kanuni za utangazaji, Tume ya Utangazaji Zanzibar imefanya ukaguzi wa leseni za utangazaji kwa vituo 81 Unguja na Pemba. Vituo vinne vimegundulika kwenda kinyume na masharti ya leseni zao na tayari vimechukuliwa hatua za kisheria. Vituo vyenyewe ni Redio Maria, Coconut Dijitali Televisheni, Zanzibar Cable na Wasafi FM.

40. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utangazaji Zanzibar imetoa jumla ya leseni **13** kwa vituo vya utangazaji zikiwemo leseni nne (4) za vituo vya televisheni, leseni nne (4) za vituo vya maudhui ya mtandaoni na leseni tano (5) za vituo vya redio. Vituo vya Televisheni vilivyopatiwa leseni ni ZBC TV, Pemba Cable Televisheni, Star Media na Mambo Cinemax, vituo vya maudhui ya mtandaoni ni ZEC online TV, Time Online, Alfath Online na Minitalk Online na vituo vya redio ni Redio Jamii Mkoani, Redio Jamii Micheweni, Elimu FM, ZBC redio, na Wasafi FM.

41. **Mheshimiwa Spika,** Tume imefanikiwa kufanya vikao vinne (4) vya Bodi ya Wakurugenzi vilivyojadili mambo mbali mbali ya kiutendaji zikiwemo shughuli za uendeshaji, kupitisha leseni za utangazaji na kuipitia rasimu ya awali ya Sera ya Tume ya Utangazaji.

42. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji umepokea kazi za uchapaji **774** kati ya **1,050** zenye thamani ya shilingi bilioni **1.35** kutoka Taasisi za Serikali na binafsi. Sambamba na hilo, Wakala umechapisha na kutangaza Magazeti Rasmi ya Serikali **171** kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Vile vile, kazi ya kuchapisha

mitihani ya kidato cha pili, darasa la saba na darasa la nne ya Baraza la Mitihani Zanzibar imefanyika kwa ufanisi, usiri na kuwasilisha kazi hiyo kwa wakati.

43. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na matumizi ya muda mrefu ya mitambo ya uchapaji inapelekea kupata hitilafu mara kwa mara na hivyo kulazimika kutumia mafundi wa ndani kutengeneza mitambo hiyo ili kazi za uchapaji ziweze kuendelea. Jumla ya mitambo tisa (9) imefanyiwa matengenezo na kubadilishwa vipuri vilivyochoka ikiwemo mtambo wa Konica Minolta, Printing, Double wire punching, Lamination, Double headlong arm stitching, HB-520A double loopwire, Semiauto strapping, Autoprint reckoner VDP 65 na Pedal stitching.

44. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Uchapaji unaendelea kutoa huduma za Bohari Kuu ya vifaa vya ofisini na kuandikia kwa taasisi za Serikali na binafsi. Jumla ya maombi **190** yenye thamani ya shilingi milioni **519** yalipokelewa na kupatiwa huduma.

Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji

45. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa chini ya Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilipangiwa kutumia **shilingi 2,000,000,000/-** kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji na kuwajengea uwezo wafanyakazi. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, mradi huu haujaingiziwa fedha.

Programu ya Maendeleo ya Vijana

46. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 7,045,799,000/-**, kati ya fedha hizo, **shilingi 645,799000/-** ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 6,400,000,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Machi 2023, jumla ya

shilingi 353,035,385/- zimepatikana sawa na asilimia **5** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana

47. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ndogo hii iliizinishiwa jumla ya **shilingi 645,799,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **shilingi 353,035,385/-** sawa na asilimia **55** zimepatikana. **Kiambatanisho 1D kinahusika.**

48. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa nazo ni hizi zifuatazo:- kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana nchini, kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, kusaidia na kuwawezesha Vijana kiuchumi, kuanzisha kituo cha Vijana kitakachowasaidia Vijana kupata huduma mbali mbali, kusaidia Mabaraza ya Vijana, kuhamasisha vijana kujiunga na Mabaraza ya Vijana na kushiriki katika shughuli za kizalendo.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha, kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana Nchini, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar, Muongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Uongozi na Uzalendo pamoja na Kufanya mapitio ya Kitini cha Kitaifa cha Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Skuli. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Shirika la UNFPA iliendesha jumla ya Mikutano nane (8) ambapo (4 Unguja na 4 Pemba) ya wadau wa maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2022/2023 ili kujadili na kupokea taarifa mbali mbali za maendeleo ya Vijana Nchini.

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa. Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka 2022, kimefanyika Tarehe 14/10/2022 katika uwanja wa CCM Sabasaba Mkoa wa Kagera na Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Jumla ya miradi **59** yenye thamani ya **shilingi 154,722,426,228.2/-** imezinduliwa na kuekewa mawe ya msingi kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru katika Mikoa mitano ya Zanzibar, ambapo miradi **23** kati ya hiyo yenye thamani ya **shilingi 109,818,558,798/-** iliyotokana na fedha za ahuweni ya UVIKO 19. Ujumbe wa mwaka 2022 ulikuwa ***''Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo, Shiriki Kuhesabiwa, Tuyafikie Maendeleo ya Taifa''.***

51. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya Vijana nchini imeendelea kuzijengea uwezo na kuziimarisha taasisi na vikundi vya vijana pamoja na kuwaunganisha na fursa za mikopo na ruzuku zilizopo hapa nchini. Kwa mwaka 2022/2023 jumla ya vikundi **285** vya kiuchumi (Unguja 163 na Pemba 122) vilitembelewa na kati ya hivyo, vikundi 41 (Unguja 37 Pemba 4) vilipatiwa msaada wa kitaalamu na malighafi. Aidha, katika ziara hiyo Idara ilifanikiwa kuanzisha jumla ya vikundi **53** vipya vya kiuchumi na kuwaunganisha kwenye huduma za mikopo. Vikundi **177** ambavyo kati ya hivyo 73 (32 Unguja na 41 Pemba) vimeshapatiwa mikopo yenye thamani ya **shilingi 669,564,219/-** (Unguja **Tzs 303,664,219/=** na Pemba **Tzs 365,900,000/-**) **(Kiambatanisho Namba 2 kinahusika)**

52. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara kupitia Mashirika ya Youth Challenge International, IRI, SOS,

PIRO na Ofisi ya ya Muheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Sahara Venture imewapatia ruzuku ya pesa taslim na vifaa vyenye thamani ya **shilingi 117,000,000/-** kwa vikundi (65) na Vijana mmoja mmoja 34. **(Kiambatanisho nambari 2 kinahusika)**

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha uratibu na ushirikiano kwa wadau mbali mbali wa Maendeleo ya Vijana katika kuandaa miradi na kuwapatia mafunzo yanayohusiana na Ujasiriamali, Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi, Uongozi na Uzalendo, Ushiriki na Ushirikishwaji, Mabadiliko ya Tabia ya nchi, Amani na Usalama na TEHAMA kwa mwaka 2022/2023. Jumla ya vijana **206,533** (Unguja **130,554** Pemba **75,979**) wakiwemo wanawake **109,177** na wanaume **97,356** wamefaidika na mafunzo hayo. ***(Kiambatanisho Namba 2A-2D vinahusika)***

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na UNICEF, UNFPA, SOS, IRI, Taasisi na wadau wengine wa maendeleo ya vijana Zanzibar imeadhimisha Siku ya Vijana Kimataifa. Shamra shamra za maadhimisho hayo zilianza tarehe 07/08/2022 kwa Bonanza la Vijana lililofanyika kuanzia Forodhani kwa maonyesho ya Makachu, Matembezi ya Vijana kuanzia kisonge hadi Uwanja wa Amaan ambapo mimi Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndiye niliekuwa Mgeni Rasmi. Aidha, kilele cha maadhimisho kilifanyika tarehe 12/08/2022 katika Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul-wakili Kikwajuni ambapo Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zaidi ya vijana 500 walishiriki katika maadhimisho hayo. Ujumbe wa maadhimisho hayo ulikuwa ni ***''Jenga Mshikamano baina ya vizazi ili kujenga Dunia ya Rika zote''.***

55. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Vijana **505** (wanaume **244**

na wanawake **261**) Unguja na Pemba waliomaliza vyuo na vyuo vikuu wamepatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo mafunzo ya uandishi wa miradi na biashara, mafunzo ya uongozi na mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya Sayansi na Teknolojia ya habari. Aidha, Baraza la Vijana Zanzibar linaendelea kuhamasisha vijana kujiunga na Baraza ambapo kwa mwaka 2022/2023 jumla ya Vijana **943** wamejiunga.

56. Mheshimiwa Spika, kupitia Baraza la Vijana Zanzibar, jumla ya Vijana **2,716** wamepatiwa elimu ya uzalendo, kuipenda nchi yao na ari ya kujitolea na hivyo kufanikiwa kushiriki katika matukio mbali mbali ya Kitaifa. Aidha, Baraza la Vijana Zanzibar liliweza kushiriki katika uzinduzi wa vituo vipya vya mafunzo ya ujasirimali Unguja na Pemba na kushiriki katika mashindano ya Mapinduzi Cup kwa timu ya nage na mpira wa mikono. Pia, Baraza lilifanya kongamano la kuadhimisha sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kushiriki katika maonesho ya biashara na wajasiriamali katika viwanja vya Maisara.

57. Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na **SOS** limeweza kuanda rasimu ya Mpango Mkakati wa Baraza la Vijana Zanzibar ya mwaka **2022/2027**. Mpango huo utakuwa ni muongozo utakaolisaidia Baraza kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Pia, Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na SOS waliweza kuandaa ligi ya Mpira wa miguu kwa lengo la kuwafanya Vijana kuwa wazalendo na kuipenda nchi yao. SOS imesaidia Baraza la Vijana Zanzibar **shilingi 51,537,500/-** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mashindao ya Mpira na kuandaa Mpango Mkakati.

58. Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kusaidia Ofisi za Baraza la Vijana Wilaya 11 Unguja na Pemba kwa kuwapatika vifaa mbali mbali vya

Ofisi ili kukuza ufanisi wa kazi katika kuleta maendeleo ya Baraza la Vijana Zanzibar. Aidha, Baraza limetembelea Miradi 13 ya Mabaraza ya Vijana Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha shughuli za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mradi wa Maendeleo ya Vijana

59. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maendeleo ya Vijana unatekelezwa ndani ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 uliidhinishiwa kutumia **shilingi 6,400,000,000/-**, hadi kufikia mwezi Machi 2023, mradi huu haujaingiziwa fedha.

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imefanikiwa kununua jengo na kufanya ukarabati kwa ajili ya kituo cha mafunzo ya Vijana katika Kijiji cha Bweleo- Wilaya ya Magharibi 'B' kupitia fedha zilizobaki katika mradi wa Pilipili. Jumla ya **shilingi 377,000,000/-** zimetumika kwa ajili ya Ununuzi na Ukarabati wa jengo hilo. Kituo hicho kimezinduliwa tarehe 5 January, 2023 na Mheshimiwa Leila Muhamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, katika shamra shamra za Sherehe za Mapinduzi.

61. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, jumla ya **shilingi 675,000,000/-** zilitumika kutoka katika Fedha za Mradi wa Maendeleo ya Vijana za mwaka 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Vijana (Youth Training Centre) katika Kijiji cha Weni Pemba ambapo jiwe la Msingi la Kituo hicho limewekwa tarehe 9/01/2023 na Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi Ofisi ya makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Vituo viwili vya Ufugaji wa Kuku vya Vijana katika Kijiji cha Mjini Ole Pemba na Kijiji cha Pangeni Unguja vimo katika hatua za mwisho za kukamilika. Vituo vyote hivyo vina lengo la kuwajengea uwezo Vijana katika maeneo ya uongozi, stadi za maisha, TEHAMA, Ushoni, Ujasiriamali na Ufugaji.

Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 15,840,971,000/**- kati ya fedha hizo, **shilingi 3,840,971,000/-** ni matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 12,000,000,000/-** kwa ajili ya Mradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 3,143,720,861/-** zimepatikana sawa na asilimia 20. Kati ya fedha hizo **shilingi 2,583,720,861/-** ni matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 560,000,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Programu Ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

63. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa inatekelezwa na Idara ya Utamaduni na Sanaa, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, (BASSFU), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 8,357,771,000/-** kati ya hizo, **shilingi 3,357,771,000/**- ni matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 5,000,000,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 2,443,096,861/-** zimepatikana sawa na asilimia 29. Kati ya fedha hizo **shilingi 2,443,096,861/-** ni matumizi ya kazi za kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **(Tafadhali angalia Kiambatanisho Namba.1D).**

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa:- kutoa elimu kuhusu matumizi bora ya lugha ya kiswahili, kuvijengea uwezo vikundi vya sanaa vya Taifa, kusajili na kukagua kazi za sanaa, kusimamia

haki za wasanii na wabunifu wa kazi za sanaa, kuratibu na kufanya matamasha mbali mbali na kufanya ukarabati wa paa la studio ya filamu.

65. **Mheshimiwa Spika,** katika harakati za kuuenzi na kuendeleza utamaduni wetu, Wizara imefanya Tamasha la 26 la Utamaduni wa Mzanzibari Unguja na Pemba na kujumuisha shughuli mbali mbali za kitamaduni kwa lengo la kuihamasisha jamii kuitambua asili yao. Maonyesho kama vile mchezo wa ngware, bidhaa za kiutamaduni, Taarab Asilia na Sanaa mbali mbali za kiasili zilifanyika. Vile vile, Idara ya Utamaduni ikishirikiana na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ziliandaa Tamasha la Kijamii (Funga Mwaka na Utamaduni) lililofanyika Disemba, 2022 katika viwanja vya Ngome Kongwe. Dhamira ya tamasha hilo ni kuutangaza utamaduni wetu (wa sanaa na bidhaa), hasa katika kipindi cha mwezi Disemba ambapo watalii wengi hutembelea visiwani humu.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekiwezesha kikundi cha Taarab cha Taifa, kikundi cha Msewe kutoka Mchanga Mdogo na Kikundi cha ngoma kutoka Mjini Ole kushiriki kwenye Tamasha la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo. Kadhalika, wasanii wanne (4) kutoka katika Jumuiya ya wasanii wa Filamu waliwezeshwa kushiriki katika mashindano ya tunzo za filamu Tanzania. Washiriki hao walifanikiwa kupata tuzo mbili (Tunzo ya Muigizaji Bora wa kike kupitia filamu ya VUTA NKUVUTE na Tunzo ya Filamu Bora ya Utamaduni kupitia filamu ya KOMBE. Idara ya Utamaduni imeendelea kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya vifaa, mavazi, vyakula na vitu vya kiasili kupitia vyombo vya habari kama vile TV, Redio na Mitandao ya Kijamii. Jumla ya vipindi 47 vya kuhamasisha jamii vimerushwa hewani.

67. **Mheshimiwa Spika,** Idara za Utamaduni za SMZ na SMT zilifanikiwa kuweka mabango ya utambulisho katika maeneo matatu (Kisiwandui, Miti Ulaya na Tawi la CCM Fumba) kupitia programu ya harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Bara la Afrika yapo maeneo kadhaa ambayo kwa namna moja au nyengine yalitumika katika harakati hizo za ukombozi Bara la Afrika.

68. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kiswahili Zanzibar linaendelea kuimarisha na kuendeleza matumizi fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar kupitia vituo vya Utangazaji na vibango. Jumla ya vipindi 63 vya Kiswahili lugha yetu vimerushwa kupitia vituo mbali mbali vya utangazaji vikiwemo ZBC TV, STAR TV, TBC 1, ZCTV, na ZBC Redio , Habari FM, Redio One, Bahari FM, BBC Redio, Morning Star Redio, Plus FM, Redio Jamii, Redio Rubondo, Citizen Redio Kenya na Redio UN. Aidha, vibango 64 vya misamiati ya lugha vimerushwa kupitia mitandao ya kijamii kwa lengo la kutoa taaluma juu ya matumizi fasaha ya misamiati ya lugha.

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili Zanzibar iliandaa Kongamano la Sita la Kiswahili la Kimataifa lililowashirikisha wadau na wataalamu wa Kiswahili wapatao 198 kutoka nchi mbali mbali zikiwemo Uganda, Rwanda, Kenya, Marekani na Tanzania. Ajenda kuu katika Kongamano hilo ni Kutathmini Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili kupitia Sayansi na Teknolojia. Baraza limefanya mikutano na Balozi mbali mbali za Tanzania nje ya nchi, kujadiliana kuhusu mpango wa ubidhaishaji wa Kiswahili. Katika mikutano hiyo vitabu 210 vikiwemo Kamusi Fasaha na Kiswahili kwa wageni vilitolewa kwa ajili ya vituo vya kufundisha Kiswahili na kuvitangaza nje ya nchi.

70. **Mheshimiwa Spika,** BAKIZA na BAKITA zimefanya maadhimisho ya Siku ya Kiswahili duniani yaliyofanyika Dar es Salaam na kutoa tunzo mbali mbali kwa waandishi wa vitabu na wahariri wa kazi za Kiswahili na kuzindua mpango mkakati wa miaka 10 wa Kitaifa wa kubidhaisha Kiswahili duniani. Sambamba na hilo, BAKIZA kwa kushirikiana na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki waliandaa Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili duniani yaliyofanyika Zanzibar tarehe 7 Julai, 2022. Lengo la Maadhimisho hayo ni kukuza na kukiendeleza Kiswahili ndani na nje ya nchi.

71. **Mheshimiwa Spika,** BAKIZA limeendelea kutangaza machapisho ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar kwa lengo la kukitangaza Kiswahili. Jumla ya machapisho 65 yameuzwa yakiwemo Kamusi ya Kiswahili Fasaha, Makamusi ya Lahaja ya Kitumbatu, Kipemba, Kimakunduchi na Kiswahili kwa Wageni. Pia, walimu wa Kiswahili 37 wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundisha Kiswahili kwa wageni.

72. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya kazi za sanaa 285 zimekaguliwa na kufanyiwa uhakiki kwa ajili ya kutolewa makosa ili ziweze kutumika hadharani. Kazi zilizohakikiwa ni maonesho ya jukwaani 15 na filamu 270 Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya wasanii 15 na vikundi 43 vya sanaa na utamaduni vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni ya mwaka 2015.

73. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari juu umuhimu wa kujisajili kwa wasanii, nidhamu ya mavazi na umuhimu wake katika kudumisha mila, silka, desturi na kulinda maadili na Utamaduni wa Mzanzibari, jumla ya vipindi 50 vimefanikiwa kurushwa hewani. Pia, Wizara imeratibu

mashindano ya uibuaji wa vipaji vya sanaa zikiwemo tenzi, ngonjera na ushairi ambapo Skuli za Msingi 12 zilishiriki. Lengo la mashindano hayo ni kuviendeleza na kuvikuza vipaji vya sanaa kwa watoto ili waweze kuwa wasanii wazuri hapo baadae.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kusimamia na kulinda haki na maslahi ya wasanii na wabunifu jumla ya kazi **504** za hakimiliki zimesajiliwa na kuingizwa katika mfumo wa Usajili. Kazi hizo ni Muziki wa Kizazi Kipya **81**, Kasida **158**, Nyimbo za Injili **135**, Muziki wa Jazz **7**, Filamu ***71***, Taarab **15**, Makala **3**, Vitabu **14**, Picha za michoro **15**, Maandishi ya Miradi **3** na Mawaidha Volume **2.** Aidha, katika kipindi hicho Afisi imesajili wabunifu wapya **45** na imetoa vyeti vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki. Kufuatia usajili huo, wasanii na wabunifu wanapata manufaa mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutambuliwa na umiliki wa kazi zao ndani na nje ya nchi na kugaiwa mirabaha.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa mirabaha, Afisi imefanikiwa kukusanya mirabaha yenye thamani ya **shilingi Milioni 113,520,908/-** na imetoa Leseni **80** kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara. Fedha hizo zilizokusanywa zinatarajiwa kugaiwa mwezi wa sita mwaka huu kwa wabunifu wa vikundi mbali mbali vya ubunifu Unguja na Pemba ambao wamesajili kazi zao katika Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar. Afisi imeandaa na kurusha hewani vipindi **12** kupitia ZBC TV, Zanzibar Cable TV, Redio Jamii ya Micheweni na Mkoani kwa ajili kutoa elimu juu ya masuala ya hakimiliki. Matokeo ya vipindi hivyo ni kuwa na jamii iliyohamasika juu ya usimamizi wa hakimiliki na matumizi halali ya kazi za hakimiliki.

76. Mheshimiwa Spika, katika kupunguza uharamia wa Hakimiliki, Afisi imefanya ukaguzi katika maeneo **245** ya watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara. Maeneo yenyewe ni Video Libraries **124**, Hoteli **72**, Taasisi za Elimu **10**, Kumbi za Burudani 10, Maduka ya Fotokopi **20**, Mikahawa **6**, Viwanja vya Kufurahishia Watoto 2 na Vyombo vya Usafiri **1**. Matokeo ya Ukaguzi huo ni watumiaji kufanya malipo ya mirabaha na kutumia kazi za hakimiliki kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa kiasi kikubwa cha uharamia hasa katika maeneo ya wauzaji wa vinasa sauti na picha vya kielektoniki. Hata hivyo, Afisi imeendelea kuwaelimisha juu ya kufuata taratibu na Sheria za kufanya biashara ya kazi za Hakimiliki.

77. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imefanya mikutano 2 ya wadau wa Hakimiliki Unguja na Pemba juu ya Urasimishaji wa Tasnia ya Hakimiliki. Sambamba na hilo, Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni (WIPO) ipo katika hatua za awali za kuandaa Sera ya Mali za Ubunifu na Mkakati wake "IP Policy and Strategy" ili kuendana na hali halisi ya maendeleo ya tasnia hii. Afisi inatambua kuwa sanaa na ubunifu sasa imekua, na ipo haja ya kuweka misingi inayoitambua kama sekta rasmi inayoweza kuwanufaisha wadau kiuchumi kama zilivyo shughuli nyingine rasmi na kuendesha sekta hii kibiashara. Kukosekana kwa Sera ya Milki Bunifu Zanzibar kunakosesha mwelekeo wa kibiashara wa wabunifu na mchango wa Tasnia hii kwa uchumi wa nchi.

78. Mheshimiwa Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Afisi imeandaa Kanuni ya Ufifilishaji wa Makosa ya Hakimiliki *(Compounding of Offences)*. Kanuni hizi pamoja na mambo mengine, zitawezesha kutoza faini ya papo kwa

papo, bila ya kwenda mahakamani punde mtuhumiwa anapokiri kosa la kukiuka Sheria ya Hakimiliki na hivyo kuepusha kwenda mahakamani ambako mtazamo wa kesi za Hakimiliki na Milki Bunifu ni finyu kutokana na uelewa mdogo wa wasimizi wa Sheria wakiwemo Polisi na Majaji.

79. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewatembelea na kuwafariji wabunifu wakongwe 25 (Unguja 15 na Pemba 10) katika maeneo yao na kuwapatia kiasi cha **shilingi 100,000/-** kila mmoja. Aidha, Afisi inaandaa kanzidata ya wasanii wakongwe itakayowezesha kazi zao kuhifadhiwa katika mfumo wa kidijitali. Kanzidata hiyo itazitambua, itazihifadhi na kutangaza wasanii na kazi zao za sanaa na ubunifu zilizowahi kuvuma na kuwa na mguso na mchango mkubwa kwa jamii ya Kizanzibari kwa wasanii wote walio hai na wale waliotangulia mbele ya haki. Kanzi data itatambua idadi ya kazi ambazo zinaingia katika matumizi ya jamii (Public Domain) na kuweza kutumika tena na wasanii na wabunifu wachanga ili kuzifanya ziweze kuiishi kama alivyofanya marehemu Bi Kidude kwa nyimbo za Siti binti Saad ambazo zinatambulika hadi sasa.

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa

80. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa unatekelezwa ndani ya Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 uliidhinishiwa kutumia **shilingi 5,000,000,000/-**, hadi kufikia mwezi Machi 2023, mradi haujaingiziwa fedha.

Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo

81. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo inatekelezwa na Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar. Kwa

mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 7,483,200,000/-** kati ya fedha hizo **shilingi 483,200,000/-** kwa kazi za kawaida na **shilingi 7,000,000,000/-** kwa Matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 700,624,000/-** zimepatikana sawa na asilimia **9**. Kati ya fedha hizo **shilingi 140,624,000/-** ni matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 560,000,000/-** kwa ajili ya Mradi wa ukarabati wa Uwanja wa michezo wa Gombani. **(angalia Kiambatanisho namba 1D kinahusika)**.

82. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa:- kuziwezesha timu kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; kuendeleza miundombinu ya michezo, kuandaa mafunzo ya waamuzi, makocha na viongozi wa michezo; kuandaa mashindano ya kombe la Mapinduzi CUP na Mashindano ya Mawizara na Kuandaa mabonaza ikiwemo bonaza la mazoezi ya viungo.

83. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza michezo nchini Wizara imefanikiwa kuwapatia mafunzo maalumu waamuzi 15 wa Mpira wa Kikapu na kusaidia vilabu na timu za Taifa kushiriki mashindano ya Kimataifa. Wizara kupitia Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar imefanikiwa kuvisaidia vyama nane (8) vya michezo kuandaa na kushiriki mashindano ya ndani na Kitaifa na vyama vitano (5) kushiriki mashindano ya kimataifa. Miongoni mwa vyama hivyo ni chama cha Mpira wa meza, chama cha mchezo wa Judo, chama cha Riadha, chama cha mchezo wa Nage, chama cha Netball, Baskeli, Basketball na mchezo wa Baseball na softball. **(Kiambatanisho nambari 3B kinahusika).**

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa michezo ya Watu Wenye Ulemavu wa mguu mmoja na mkono mmoja, Wizara imefanikiwa kulisaidia Shirikisho la mchezo huo kushiriki mashindano ya Kitaifa yaliyofanyika Arusha. Aidha, Shirikisho la michezo ya Viziwi Zanzibar (SHIMIVIZA) limesaidiwa kuandaa Bonanza kwa ajili ya shamra shamra ya kuadhimisha siku ya Viziwi Duniani. Kwa kutambua haki na wajibu wa kila mtu katika michezo, Wizara imeweza kusimamia uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Meza, chama cha kuogolea Zanzibar na Mpira wa Kikapu katika hali ya amani na uadilifu mkubwa.

85. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuanzisha mchezo wa Ngumi (Boxing) baada ya kuzuiliwa kwa muda mrefu kuchezwa na kufanyika kwa mashindano hayo hapa Zanzibar. Kwa sasa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limeunda uongozi wa muda kwa ajili ya kusimamia taratibu za kisheria za kuusajili rasmi mchezo huo. Usajili umekamilika na maandalizi ya kuanza mashindano ya mchezo huo yanaendelea.

86. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanikisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yalifanyika Zanzibar Januari, 2023. Jumla ya timu **6** kutoka Zanzibar, timu **5** kutoka Tanzania Bara na timu **1** kutoka Burundi zilishiriki mashindano hayo. Timu ya Mlandege kutoka Zanzibar iliibuka mshindi na kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi kwa mwaka 2023. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na chama cha Mazoezi ya viungo Zanzibar (ZABESA) imefanikisha kuandaa Tamasha la siku ya mazoezi ya viungo Kitaifa liliofanyika katika kiwanja cha Gombani ya Kale kisiwani Pemba. Tamasha hilo lilifanyika tarehe 1, Januari, 2023 na jumla ya vilabu 137 vilishiriki, kati ya hivyo 90 kutoka Unguja, 30 kutoka Pemba na 17 kutoka Tanzania Bara. Katika Tamasha hilo Mgeni rasmi alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kauli mbiu kwa mwaka 2023 ni***" Shughulisha mwili wako, Acha kubweteka, Afya ni utajiri".***

87. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Idara ya Michezo imefanikisha mashindano ya Mawizara, Mashirika na Taasisi za kiserikali katika mchezo wa mpira wa miguu, mchezo wa kuvuta kamba na mchezo wa riadha. Jumla ya timu 36 za mpira wa miguu (Unguja 24 na Pemba 12), timu 5 za mchezo wa kuvuta kamba na timu 6 za mchezo wa riadha zilishiriki. Timu za michezo ya riadha na kuvuta kamba ilikua na washiriki wa kike na wakiume. Kwa upande wa mshindi wa mashindano hayo, timu ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutoka Unguja iliibuka mshindi wa mchezo wa mpira wa miguu dhidi ya timu ya Wizara ya Afya kutoka Pemba ambapo kwa mara ya kwanza mashindano haya yaliwakutanisha washindi wa mpira wa miguu bingwa wa kanda ya Unguja na bingwa kanda ya Pemba walicheza na kupatikana mshindi wa Zanzibar.

88. Mheshimiwa Spika, timu ya Shirika la Bandari ilipata ushindi wa kuvuta kamba kwa wanaume na wanawake. Mshindi wa kwanza riadha mita 100 alitoka Mamlaka ya viwanja vya ndege kwa wanaume na wanawake. Mshindi wa kwanza riadha mita 200, 400 na 800 alitoka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa wanaume wakati kwa upande wanawake mshindi alitoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Mashindano hayo yaliibua hamasa kwa wachezaji na kuimarisha ushirikiano, udugu na umoja miongoni mwa wafanyakazi wa Mawizara, mashirika na Taasisi za Serikali.

89. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya michezo, Wizara kupitia Idara ya Michezo imefanya ukarabati katika uwanja wa Amaan na Mao ze Dong kwa kuweka 'grill' katika vibanda vya kuuzia tiketi, madirisha

ya VIP na 'control room', kutengeneza mfumo wa vyoo vya VIP, kupaka rangi na kuvifanyia matengenezo vipooza hewa, kutengeneza ngazi ya kupandia waandishi wa habari, kujenga ukuta wa fensi ya uwanja, kuweka zulia na vitasa vipya kwenye vyumba vya wachezaji.

90. Mheshimiwa Spika, pia, Wizara inaendelea kuufanyia ukarabati mkubwa uwanja wa Gombani ili kurejesha hadhi na muonekano wa uwanja huo. Sambamba na hilo, Wizara imepokea kifaa cha kupima hali ya hewa ya uwanja (Air Quality Sensor) ambacho kimefungwa katika uwanja wa Amaan. Kifaa hichi ni msaada kutoka Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) na Taasisi ya Mazingira ya Sweden (SEI) kwa kushirikiana na Shirikisho la Riadha la Kenya. Kifaa hicho kitasaidi kujua hali ya uwanja iwapo unafaa kuchezewa au haufai kutokana na hali ya hewa iliopo. Zanzibar ni nchi ya nne kuwa na kifaa hicho Barani Afrika.

91. Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kufunga mkataba na Shirika la Kimataifa la Ujerumani (GIZ) wanao fadhili ujenzi wa viwanja vinne vya michezo midogo midogo (6 in 1) Unguja na Pemba. Maeneo yatakayojengwa viwanja hivyo ni pamoja na Mkototoni na Mnazimmoja kwa Unguja na Mchangamdogo na Kangani kwa upande wa Pemba. Maandalizi ya Ujenzi wa viwanja hivyo umeanza mwezi Mei 2023. Katika hatua nyengine, Idara ya Michezo kwa kushirikiana na Kampuni ya Refocus Afrika inaendelea kusimamia mafunzo ya mchezo wa mpira wa kikapu kwa walimu wa timu za watoto hapa Zanzibar. Mafunzo yanaendeshwa na wakufunzi kutoka Marekani na yanalenga kuwafundisha walimu ili baadae kuanzisha ligi ya watoto ya mchezo wa kikapu.

Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo

92. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo unatekelezwa ndani ya Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 uliidhinishiwa kutumia **shilingi 7,000,000,000/-** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Michezo. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, mradi umeingiziwa **shilingi 560,000,000/-** sawa na asilimia **8** kwa ajili ya Ukarabati wa Uwanja wa Gombani ambao ulitengewa jumla ya **shilingi 2,800,000,000/-**.

Programu ya Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Vijana, Utamaduni na Michezo

93. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii iliidhinishiwa **shilingi 3,215,030,000/-** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2023, jumla ya **shilingi 2,324,353,125/-** zilipatikana sawa na asilimia **72**. Programu hii inaundwa na programu ndogo ndogo tatu ambazo ni :- Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara na Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Wizara Pemba.

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

94. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,137,000,000/-** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2023 imefanikiwa kupata **shilingi 1,515,987,425/-** sawa na asilimia **71. (kiambatanisho namba1D kinahusika)**

95. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa ambazo ni:- kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vifaa vya ofisi na vitendea kazi, kuwajengea uwezo wafanyakazi, kulipa stahiki za wafanyakazi, kuandaa mpango wa manunuzi, kuratibu vikao vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi.

96. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani na vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Wafanyakazi 52 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao 25 wanaume na 27 wanawake na Wafanyakazi 26 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi wakiwemo wanaume 17 na wanawake 9. Pia, Wafanyakazi 62 wamepatiwa mafunzo kuhusiana na masuala mtambuka yakiwemo kukabiliana moto, kupambana na rushwa, UKIMWI na udhalilishaji. Mafunzo yote haya yalilenga kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya wafanyakazi ya kila siku.

97. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia watendaji vitendea kazi na vifaa mbali mbali vya kazi kwa ajili ya kuongeza bidii na kuimarisha ufanisi wa kazi. Pia, wafanyakazi wote wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, fedha za likizo, haki ya mapumziko baada kujifungua mtoto kwa mama na baba. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo, mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano na mpango wa manunuzi 2022/2023.

98. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeratibu ziara za viongozi wakuu wa Wizara ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara na kuimarisha

ushirikiano na wadau mbali mbali wa Wizara. Mikutano ya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na vikao vya bodi ya zabuni vimeratibiwa kwa lengo la kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Pia, Idara imefanikiwa kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti za ukaguzi wa fedha kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma yanafanyika kwa usahihi.

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

99. Mheshimiwa Spika, programu ndogo hii ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka 2022/2023 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 160,800,000/-** na hadi kufikia mwezi Machi 2023 imefanikiwa kupata jumla ya **shilingi 44,000,000/-** sawa na asilimia **27**. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D).**

100. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuandaa mipango na kutayarisha bajeti ya Wizara, kuratibu na kusimamia Sera za Wizara, kufanya tafiti za Wizara, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi na programu za Wizara, kuandaa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuziwasilisha, kuratibu vikao na ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na Kuratibu na Kusimamia vikao vya Ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

101. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kutayarisha mpango mkakati wa miaka mitatu, mpango wa utekelezaji wa mwaka mmoja, mpango wa matumizi (MTEF) wa muda wa kati, kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika taasisi zinazo

husika. Aidha, Wizara imetayarisha hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

102.Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kufanya utafiti kuhusu mchango wa ngoma za asili na jitihada za kuzifufua katika Wilaya 11 za Zanzibar. Utafiti huu ulitumia njia ya dodoso kukusanya maoni kupitia makundi ya wazee na vijana ambapo jumla ya wahojiwa **330** wakiwemo **179** wanaume na **151** wanawake. Matokeo ya utafiti huo yamebaini zaidi ya ngoma 94 zimetoweka (kufa) na ngoma 24 tu ndizo ambazo ziko hai ingawa nazo ziko hatarini kutoweka. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwepo kwa mwamko mdogo wa wanajamii hususan vijana katika kuziendeleza Ngoma za Asili.

103.Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara imefanikiwa kufanya utafiti kuhusu kuchunguza ukubwa wa eneo la watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara Zanzibar. Utafiti huu ulitumia njia ya dodoso kukusanya maoni kupitia Vituo vya Utangazaji vya Serikali na binafsi, Mahoteli, Kumbi za Burudani na Sherehe, Watumiaji wa kazi za maandishi, maduka ya kukodisha CD na Maduka ya Fotokopi. Jumla ya wahojiwa **300** wakiwemo wanaume **270** na wanawake **30** walishiriki katika kutoa maoni hayo. Matokeo ya utafiti huo yamebaini kuwa wafanya biashara wengi wanaotumia kazi za hakimilki wanakwepa kulipa kodi za biashara wanazofanya kwa kisingizio cha ugumu wa biashara. Aidha, utafiti umebaini kuwepo kwa utitiri wa lesseni kwenye biashara moja sambamba na viwango vya ada ya lesseni ya hakimiliki kuwa kubwa bila ya kuzingatia ukubwa wa matumizi na maeneo yanayofanyia biashara wenyewe.

104.Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa miradi, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi

iliyofuatiliwa ni ukarabati wa kituo cha mafunzo ya vijana Bweleo, Ujenzi wa mabanda ya kuku Pangeni kwa upande wa Unguja, na Ukarabati wa Uwanja wa Gombani, Ujenzi wa Mabanda ya Kuku Mjini Ole na Ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Vijana Weni kwa Upande wa Pemba. Miradi hii imo katika programu ya uimarishaji viwanja vya michezo na programu ya maendeleo ya vijana.

105.Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu vikao vya Kamati za Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kutekeleza majukumu yao ya kusimamia utekelezaji wa Serikali kwa upande wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Vile vile, Wizara imeratibu ziara ya Kamati ya Ustawi wa Jamii na Kamati ya Kanuni ndogo ndogo ya Baraza la Wawakilishi Unguja, Pemba na Dar es Salaam katika kufanya ufuatiliaji wa shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara.

106.Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu vikao viwili vilivyofanyika Zanzibar na kushiriki vikao vitatu vilivyofanyika Dar es Salaam na Dodoma vya ushirikiano baina ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar na taasisi zinazoshabiihiana kiutendaji zilizo chini ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Sambamba na hilo, Idara ya Mipango imeshiriki katika kikao cha ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na DRC kilichofanyika Dodoma na Kikao cha ushirikiano baina ya Tanzania na Uganda kilichofanyika Dodoma. Lengo la vikao vyote hivyo ni kujenga ushirikiano katika utendaji wa kazi za Serikali kwa lengo la kuleta usawa, amani na umoja.

107.Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya mikutano miwili ya wadau wa sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa lengo la kukusanya maoni juu ya uandaaji wa mpango mkakati wa Wizara. Jumla ya washiriki 60 Unguja na

Pemba walishiriki na kutoa maoni yao. Vile vile, Idara imefanikiwa kufanya vikao vitatu (kila robo mwaka) vya maafisa Mipango wa taasisi zilizomo chini ya Wizara. Lengo la vikao hivi ni kutoa maelekezo katika kuandaa mipango na utekelezaji wa shughuli za programu za Wizara.

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba

108. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 917,230,000/-** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2023, imefanikiwa kupata jumla ya **shilingi 764,365,700/-** sawa na asilimia **83 (Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D).**

109. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2022/2023, shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba, kuwajengea uwezo wafanyakazi na mazingira mazuri ya kazi, kulipa stahiki za wafanyakazi, kutoa uelewa kuhusiana na masuala mtambuka.

110. Mheshimiwa Spika, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuratibu vikao 6 vya Kamati za Baraza la Wawakilishi na kuratibu zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya tafiti za Wizara ikiwemo utafiti wa kubaini ukubwa wa maeneo ya watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara. Kwa mafanikio makubwa, Ofisi imeratibu bonaza la michezo lililojumuisha michezo mbali mbali ikiwemo Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu na Mpira wa Pete kwa lengo la kuihamasisha jamii kuendeleza michezo na kujenga afya zao.

111.Mheshimiwa Spika, Ofisi Kuu Pemba inaendelea kufuatilia na kusimamia ujenzi wa mabanda ya kuku Mjini Ole na Kituo cha Maendeleo ya Vijana kilichopo Weni, sambamba na kusimamia ukarabati wa uwanja wa Gombani kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji na ufanisi wa miradi ya Wizara kwa upande wa Pemba. Watendaji wa Wizara Pemba wamefanya vikao mbali mbali na wadau wakiwemo wenyeviti na makatibu wa vyama vya michezo, viongozi wa vikundi vya sanaa, wenyeviti na makatibu wa mabaraza ya vijana ya Shehia na Wilaya. Mikutano hiyo ilikuwa na lengo la kujadili changamoto na kutafuta suluhisho la masuala yanayohusu vijana, sanaa na michezo kwa ujumla.

112.Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi na kutoa huduma za kiutawala, Wizara imefanikiwa kulipa posho baada ya masaa ya kazi, malipo ya likizo, haki ya mapumziko baada ya kujifungua mama na baba, haki ya ubani wa ufiwa na malipo ya safari kikazi. Mfanyakazi 1 amepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 3 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na wafanyazi 32 wamepatiwa mafunzo ya awali kazini (induction course). Pia, Wizara kwa upande wa Pemba inaendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia watendaji huduma za vitendea kazi na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

113.Mheshimiwa Spika, watendaji wa Ofisi Kuu Pemba wamefanya vikao vya wafanyakazi na vikao vya Kamati Tendaji vikiwa na lengo la kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kukumbushana haki na wajibu wa kila mfanyakazi. Aidha, Ofisi inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo, mpango wa manunuzi na mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

F. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

114. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imetengewa jumla ya **shilingi 51,939,984,000/-**. Kati ya fedha hizo **shilingi 17,661,930,000/-** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 34,278,054,000/-** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. **(kiambatanisho nambari 1F-1G vinahusika)**

115. Mheshimiwa Spika, katika fedha za matumizi ya kazi za kawaida **shilingi 12,490,097,000/-** ni kwa ajili ya mishahara, kati ya fedha hizo **shilingi 5,455,200,000/-** ni mishahara ya Idara zilizomo ndani ya Wizara na **shilingi 7,034,897,000/-** ni mishahara kwa taasisi zinazopokea ruzuku.

116. Mheshimiwa Spika, jumla ya **shilingi 5,171,834,000/-** ni fedha za matumizi mengineyo, kati ya hizo **shilingi 2,166,084,000/-** ni matumizi mengineyo ya Idara zilizomo ndani ya Wizara na **shilingi 3,005,750,000/-** kwa taasisi zinazopokea ruzuku. **(kiambatanisho 1F-1G vinahusika)**

117. Mheshimiwa Spika, Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 875,997,000/-** ambazo zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia vyanzo mbali mbali na shilingi **16,071,000,000/-** ni makusanyo yanayokusanywa nakutumiwa na Taasisi husika **(kiambatanisho 1H na 1I vinahusika)**

G. MAENEO YA VIPAOMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

118. Mheshimiwa Spika, Wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaombele kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Vipaombele hivyo ni kama vifuatavyo:-

i. Kufanya mageuzi ya kisera na kisheria katika kusimamia masuala ya habari na kujengea uwezo Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji kwa kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa;

ii. Kuimarisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) na Z-MUX kwa kuzipatia vifaa ikiwemo gari maalumu za kurushia matangazo (OB Van), na wataalamu ili kuweza kutayarisha na kurusha hewani vipindi vyenye ubora na kuimarisha wigo wa upatikanaji na matangazo yake;

iii. Kuimarisha Shirika la Magazeti ya Serikali la Zanzibar kwa kuwapatia jengo jipya la ofisi na kuendelea kusambaza nakala za Magazeti ya Zanzibar Leo, Zanzibar Mail, Zasport kutoka mikoa kumi na moja Tanzania Bara hadi kufikia mikoa ishirini na tano pamoja na kuyauza magazeti kwa njia ya mtandando ili yasomwe duniani kote;

iv. Kuimarisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kwa kuwapatia jengo jipya la kuwekea mitambo na bohari la vifaa, pamoja na kupatiwa mashine na vifaa vya kisasa vya uchapishaji na kuongezewa mtaji wa kuliwezesha kutoa huduma za vifaa vya uchapishaji na kujiendesha;

v. Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana nchini na kuwawezesha vijana kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa;

vi. Kuratibu na kuyajengea uwezo mabaraza ya Vijana Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa;

vii. Kuendeleza, kukuza na kueneza Kiswahili na kuwa bidhaa katika matumizi ya shughuli za taaluma zikiwemo za uandishi, uchapishaji, ukalimani na kuwa moja ya lugha iliyo rasmi inayozungumzwa na kutambulika katika mashirika na mikutano ya kikanda na kimataifa;

viii. Kuhamasisha sekta binafsi kutambua na kulinda mila na utamaduni;

ix. Kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa matumizi ya mavazi, vifaa, vyakula na vitu vya kiasili ili kulinda, kuendeleza na kurithisha amali za kitamaduni kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho;

x. Kuandaa utaratibu wa kuzitambua, kuziendeleza na kuzisajili kazi za kiutamaduni zitakazozalishwa nchini na kuziongeza thamani pamoja na kulinda hakimiliki za ubunifu kisheria;

xi. Kuhakikisha kunakuwa na miundombinu ya sanaa katika maeneo mbali mbali pamoja na kuendeshwa kwa vikundi vya sanaa kwa misingi ya uwazi na uwajibikaji na kwa kufuata sheria na kanuni;

xii. Kuendelea kusimamia na kulinda haki na masilahi ya wasanii pamoja na Kuendelea kuimarisha mfumo wa kuibua vipaji vya wasanii na kuwatunza na kuwaenzi wasanii wakongwe waliohai na waliofariki; na

xiii. Kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya michezo kwa kufanya ukarabati mkubwa wa Kiwanja cha Michezo cha Amaan na Gombani na kujenga viwanja vya michezo vya kisasa kwa kila Wilaya.

H. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

119. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inakadiriwa kutumia jumla ya **shilingi 51,939,984,000/-**,kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu nne kama ifuatavyo:-

a. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji (PJ0301) **ni shilingi 9,612,311,000/-**;

b. Programu ya Maendeleo ya Vijana (PJ0302) ni **shilingi 628,598,000/-**;

c. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (PJ0303) ni **shilingi 38,156,150,000/**-; na

d. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (PJ0304) ni **shilingi 3,542,926,000/-**.

Programu kuu: PJ 0301 maendeleo ya habari, utangazaji na uchapaji

120. Mheshimiwa Spika, Lengo la Programu hii ni Kuongezeka kwa Upatikanaji na Usambazaji wa Habari za Kijamii, Kisiasa, Kiutamaduni na Kiuchumi kwa wananchi kwa wakati. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwa wananchi wanapata huduma na kutumia habari zenye kiwango bora kwa maslahi yao na Taifa. Programu hii imepangiwa kusimamia Programu Ndogo mbili kama ifuatavyo:-

Programu Ndogo: SJ030101 Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

121. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar (SMS) na Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX). Jukumu la msingi la programu hii ni kufikisha habari za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi kwa wananchi kwa wakati.

122. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa katika programu ndogo hii ni utoaji wa Taarifa, Picha, Makala, Filamu na Sinema; Urushaji wa vipindi na Matangazo kupitia TV na Redio, Utoaji wa Magazeti na Usambazaji wa Maudhui ya Utangazaji.

123. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa habari, picha, makala na filamu za matukio mbali mbali ya kiserikali na kuziwasilisha kwa jamii ili jamii iwe na uelewa wa matukio na shughuli za Serikali;

ii. Kuandaa mafunzo ya Maafisa habari na mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. Kulitangaza Shirika la Utangazaji Zanzibar kupitia vyombo vya habari mbali mbali vya Kitaifa na Kimataifa;

iv. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia iliyopo;

v. Kutoa taarifa kwa jamii kupitia vyombo vya habari vikiwemo tv na redio;

vi. Kuendelea kuimarisha Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) kwa kuipatia vifaa vya kisasa na huduma muhimu ili kuendendana na wakati uliopo;

vii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui;

viii. Kuimarisha shughuli za uchapishaji na usambazaji wa gazeti ili kuongeza mapato kwa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar; na

ix. Kurekebisha Sera na Sheria za Shirika la Magazeti ya Serikali.

124. Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 7,231,011,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu Ndogo: SJ030102 Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji

125. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar. Jukumu la msingi katika programu hii ni kudhibiti na kusimamia vituo na shughuli za utangazaji kupitia Sera, Sheria za Habari na Utangazaji. Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika programu hii ni kudhibiti na kusimamia vituo vya utangazaji, kusimamia shughuli za uchapaji, upatikanaji wa vifaa vya ofisi na kuandikia na kudhibiti na kusimamia shughuli za Utangazaji.

126. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya programu shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kusimamia vyombo vya habari kwa kutoa vibali vya upigaji wa picha kwenye maeneo ya Zanzibar, vibali vya uanzishwaji wa gazeti na majarida, mawakala wa habari na kutoa vitambulisho kwa waandishi wa habari wanaofanya kazi katika vyombo vya habari vya umma na binafsi;

ii. Kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji Zanzibar kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji;

iii. Kuwajengea uelewa wadau wa utangazaji Zanzibar ili kufuata sheria na maadili ya habari;

iv. Kuimarisha wigo wa masoko kwa lengo la kuongeza mapato na kumuwezesha Wakala wa Uchapiji wa Serkali kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi; na

v. Kuendelea kutoa huduma za uchapaji pamoja na kuimarisha Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na vya Kuandikia.

127. Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 2,381,300,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Program Kuu: PJ0302 Maendeleo ya Vijana

128. Mheshimiwa Spika, lengo kuu la programu hii ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana, kuwawezesha kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii

na kisiasa kupitia programu mbali mbali. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuongezeka idadi ya ajira kwa vijana. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 628,598,000/-** na imepangiwa kusimamia programu ndogo moja.

Programu Ndogo: SJ030201 Maendeleo ya Vijana

129. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar ambapo jukumu la msingi katika programu hii ni kuwawezesha vijana ili kuimarisha ustawi wao na kujenga uchumi na maendeleo ya jamii. Huduma zinazotarajiwa kutolewa katika programu hii ni Kuratibu na Kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana, Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Kusimamia Uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana.

130. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya vijana;

ii. Kuimarisha Vituo vya Mafunzo kwa Vijana pamoja na kuanzisha vipya;

iii. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

iv. Kufanya ufatiliaji kwa Mabaraza ya Vijana Wilaya na Shehia pamoja na kuyasaidia Mabaraza ya Vijana Taifa, Wilaya na Shehia; na

v. Kutekeleza programu za elimu na malezi kwa Vijana pamoja na mikakati ya kujenga moyo wa Uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao;

131.Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 628,598,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu Kuu: PJ0303 Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

132.Mheshimiwa Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa ya Zanzibar zinaenziwa, wasanii wanaendelezwa ili kupunguza umaskini, kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga amani, utulivu, urafiki, ajira na kujenga afya kwa jamii. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni, kukuwa na kuendelea kwa Lugha ya Kiswahili na kukuwa kwa Michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 38,156,150,000/- na itasimamia programu ndogo mbili.

Programu Ndogo: SJ030301 Uimarishaji Uhifadhi, Uendelezaji wa Utamaduni Sanaa na Ubunifu

133.Mheshimiwa Spika, programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Utamaduni, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili Zanzibar na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Jukumu la msingi la programu hii ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni, sanaa na ubunifu Zanzibar.

134.Mheshimiwa Spika, huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa, Kuendeleza Matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili, Kusajili na Kusimamia kazi za Hakimiliki, Ukaguzi wa Filamu na Sanaa za Maonyesho na Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha kwa wamiliki wa hakimiliki.

135. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya programu hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na kuyaendeleza matamasha ya kijamii;

ii. Kuimarisha Studio ya Filamu na Muziki Raha leo kwa kuipatia vifaa ili iweze kuzalisha kazi zenye ubora katika ladha ya Kitaifa na Kimataifa;

iii. Kuendelea na ukaguzi wa Filamu na kazi za Sanaa za Maonyesho;

iv. Kutoa elimu kwa Wasanii juu ya umuhimu wa kujisajili pamoja na umuhimu wa Mikataba na Urasimishaji wa kazi za Sanaa;

v. Kukusanya Mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara na kuigawa mirabaha hiyo kwa wamiliki wa hakimili;

vi. Kuandaa Programu za kutoa elimu kwa wadau wa Hakimiliki (Copyright Respect Jurisdction Program);

vii. Usimamizi na usambazaji wa matumizi ya Kiswahili fasaha kwa wageni na wenyeji kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; na

viii. Kuandaa kongamano la Saba la Kiswahili la Kimataifa.

136. Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji Utamaduni na Sanaa iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 3,456,496,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu Ndogo: SJ030302 Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo

137. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji Michezo inatekelezwa na Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar. Jukumu la programu hii ni kusimamia maendeleo ya micheo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Ukuzaji na Uendelezaji Michezo na Usimamizi wa shughuli za vyama vya Michezo kupitia Sheria ya Baraza la Michezo.

138. **Mheshimiwa Spika**, ili programu hii itekelezwe kwa ufanisi shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuwezesha timu za Taifa kushiriki mashindano ya Kikanda na Kimataifa;

ii. Kuimarisha na kujenga miundombinu ya michezo;

iii. Kuvisaidia vyama vya michezo kuandaa na kushiriki katika mashindano ya ndani na Kitaifa;

iv. Kuvisaidia vyama vya michezo vya Watu Wenye Ulemavu kushiriki katika michezo;

v. Kuvisaidia vyama vya vya michezo kufanya marekebisho ya katiba zao pamoja na chaguzi; na

vi. Kutoa mafunzo ya kuwajengea uelewa wa matumizi ya katiba na kanuni na miongozo mbali mbali ya michezo kwa viongozi wa vilabu.

139. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 34,699,654,000/-,** kati ya hizo **shilingi 421,600,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 34,278,054,000/-** kwa Miradi ya Maendeleo.

Programu Kuu: PJ0304 Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

140.Mheshimiwa Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 3,542,926,000/-** na itasimamia programu ndogo tatu.

Programu Ndogo: SJ030401 Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

141.Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Huduma ambazo inayotarajiwa kutolewaa ni Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti.

142.Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya programu hii kwa ufanisi shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuratibu Maandalizi, Mapitio na Machapisho ya Sera za Wizara;
ii. Kuratibu na kusimamia ufanyaji wa tafiti za Kiutendaji za Wizara;
iii. Kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
iv. Kuratibu na Kufuatilia utekelezaji wa Programu za Wizara;
v. Kuratibu na Kusimamia vikao vya Ushirikiano baina ya SMZ na SMT; na
vi. Kuweka mazingira bora ya kazi kwa kutoa huduma ya vifaa, vitendea kazi vya ofisi na kulipa stahiki za wafanya kazi.

143. Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 168,000,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu Ndogo: SJ030402 Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

144. Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa Wizara. Lengo Mahsusi la programu hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa wafanyakazi wa Wizara. Huduma inayotarajiwa kutolewa ni kuwajengea uwezo wafanyakazi na kueka mazingira bora ya kazi.

145. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia programu hii ndogo inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu;
ii. Kuimarisha vitengo vya Wizara kwa kuvipatia huduma muhimu;
iii. Kuongeza uelewa kwa wafanyakazi katika masuala ya UKIMWI, Unyanyapaa na Rushwa; na
iv. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuipatia Ofisi vifaa na huduma.

146. Mheshimiwa Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 2,224,934,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Programu Ndogo: SJ030403 Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

147. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Lengo la programu ndogo hii ni kuhakikisha mipango, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu Pemba na kuwajengea uwezo wafanyakazi, kueka mazingira bora ya kazi na kulipa stahiki za wafanyakazi.

148. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii kwa ufanisi shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuratibu shughuli za tafiti Pemba;

ii. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia vifaa wafanya kazi wa ofisi Kuu Pemba;

iii. Kuratibu, kusimamia na Kutathmini Miradi na Shughuli za Ofisi Kuu Pemba; na

iv. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya mikakati ya kupambana na Rushwa, UKIMWI, Matumizi Mabaya ya Dawa za Kulevya na Ukatili wa Watoto.

149. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,149,992,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

I. SHUKRANI

150.Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hotuba yangu naomba kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi mbali mbali anazoendelea kuchukuwa katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na kuisimamia vyema Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa kuhakikisha inatekelezwa kikamilifu.

151.Mheshimiwa Spika, itakuwa sikufanya jambo jema nikiacha kuwapongeza watendaji wangu wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Nikianza na Katibu Mkuu wangu Ndugu Fatma Hamad Rajab, Afisa Mdhamini Pemba ndugu Mfamau Lali Mfamau, Wakurugenzi, Makamishna, Makatibu Watendaji na wafanyakazi wote kwa namna wanavyonipa ushirikiano mkubwa na wepesi wa kuiongoza Wizara hii katika kutimiza Malengo yake.

152.Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waandishi wa Habari wote, Vijana wote, Wanamichezo, Wasanii na Wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Pia, shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vya kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Vijana, Utamaduni na taarifa za michezo.

153.Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuzishukuru Wizara zote na Taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali kwa ushirikiano mzuri mnaotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Wizara.

154.Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa naomba nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika ya kimaendeleo ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa

China, Afrika ya Kusini, Msumbiji, Rwanda, Shirika la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), UNICEF, UNESCO, Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni (WIPO), ARIPO, PBZ, CRDB, NMB, Equity Bank, NIC, ZAT, BANDARI, ZURA, SUZA, AZAM Media, Coaches Across Continents, Youth Challenge International, TAMWA, JUWAHAZA, TAHA, S.O.S, CHARITY SCHOOL BWEJUU, Tume ya Utangazaji Tanzania, Jukwaa la Wahariri, Baraza la Habari, Asasi za Kiraia zinazosaidia vijana pamoja na Washirika wote wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

J. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

155. Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya **shilingi 51,939,984,000/-.** Kati ya fedha hizo **shilingi 17,661,930,000/-** kwa kazi za kawaida na **shilingi 34,278,054,000/-** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu lidhinishe makusanyo ya mapato ya **shilingi 875,997,000/-** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

156. Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa nawaomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

157. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (MBM),
Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo
Zanzibar.

VIAMBATANISHO

KIAMBATISHO NAMBA 1 A

FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

NO	IDARA	MAELEZO	BAJETI 2022/2023	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULY -MARCH 2022/2023	ASILIMIA
1	Afisi Kuu Pemba	Mishahara			101%
			657,230,000	661,573,700	
		Matumizi Mengineo	260,000,000	102,792,000	40%
	JUMLA		**917,230,000**	**764,365,700**	**83%**
2	Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	160,800,000	44,000,000	27%
	JUMLA		**160,800,000**	**44,000,000**	**27%**
3	Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	1,027,000,000	1,082,560,025	105%
		Matumizi Mengineo	1,110,000,000	433,427,400	39%
	JUMLA		**2,137,000,000**	**1,515,987,425**	**71%**
4	Maendeleo ya Vijana	Mishahara	148,899,000	156,085,385	105%
		Matumizi Mengineo	145,000,000	53,575,000	37%
	JUMLA		**293,899,000**	**209,660,385**	**71%**
5	Idara ya Utamaduni na Sanaa	Mishahara	1,728,471,000	1,687,756,710	98%
		Matumizi Mengineo	445,000,000	133,000,000	30%
	JUMLA		**2,173,471,000**	**1,820,756,710**	**84%**
6	Idara ya Michezo	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	310,000,000	99,000,000	32%
	JUMLA		**310,000,000**	**37,000,000**	**12%**
7	Idara ya Habari Maelezo	Mishahara	462,500,000	469,610,245	102%
		Matumizi Mengineo	510,000,000	93,500,000	18%
	JUMLA		**972,500,000**	**563,110,245**	**58%**

	Jumla ya Mishahara		**4,024,100,000**	**4,057,586,065**	**101%**
	Jumla ya Matumizi Mengine		**2,940,800,000**	**959,294,400**	**33%**
	Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku		**6,964,900,000**	**5,016,880,465**	**72%**
	TAASISI ZA RUZUKU				
1	Baraza la Vijana Zanzibar	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo			41%
			351,900,000	143,375,000	
			351,900,000	**143,375,000**	**41%**
2	Afisi ya Msajili na Hakimiliki	Mishahara	204,200,000	206,351,680	101%
		Matumizi Mengineo	431,600,000	137,763,871	32%
	JUMLA		**635,800,000**	**344,115,551**	**54%**
3	Baraza la Kiswahili Zanzibar	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	303,900,000	174,524,000	57%
	JUMLA		**303,900,000**	**174,524,000**	**57%**
4	Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	244,600,000	103,700,600	42%
	JUMLA		**244,600,000**	**103,700,600**	**42%**
5	Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	173,200,000	41,624,000	24%
	JUMLA		**173,200,000**	**41,624,000**	**24%**
6	Tume ya Utangazaji	Mishahara	220,800,000	335,516,670	152%
		Matumizi Mengineo	163,500,000	134,372,000	82%
	JUMLA		**384,300,000**	**469,888,670**	**122%**
7	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	2,173,800,000	2,552,669,430	117%
		Matumizi Mengineo	2,203,000,000	482,919,000	22%
	JUMLA		**4,376,800,000**	**3,035,588,430**	**69%**
8	Shirika la Magazeti	Mishahara	557,600,000	638,701,005	115%
		Matumizi Mengineo	726,100,000	166,000,000	23%
	JUMLA		**1,283,700,000**	**804,701,005**	**63%**

	JUMLA		**1,283,700,000**	**804,701,005**	**63%**
9	kampuni ya Uunganisha Maudhui (ZMUX)	Mishahara	-	-	-
		Matumizi Mengineo	421,000,000	134,508,000	32%
	JUMLA		**421,000,000**	**134,508,000**	**32%**
10	Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP)	Mishahara	1,204,500,000	1,394,530,085	116%
		Matumizi Mengineo	-	-	-
	JUMLA		**1,204,500,000**	**1,394,530,085**	**116%**
	Jumla ya Mishahara ya Ruzuku		**4,360,900,000**	**5,127,768,870**	**118%**
	Jumla ya matumizi mengineo ya ruzuku		**5,018,800,000**	**1,518,786,471**	**30%**
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**9,379,700,000**	**6,646,555,341**	**71%**
	Jumla ya Mishahara kwa Wizara		**8,385,000,000**	**9,185,354,935**	**110%**
	Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara		**7,959,600,000**	**2,478,080,871**	**31%**
	JUMLA KUU YA WIZARA MATUMIZI YA KAWAIDA (A)		**16,344,600,000**	**11,663,435,806**	**71%**
	Miradi ya Maendeleo				
1	Mradi wa Maendeleo ya Vijana		6,400,000,000	-	0%
2	Uimarishaji wa viwanja vya Wilaya SMZ		4,000,000,000	560,000,000	14%
3	Ujenzi wa Viwanja vya Nje na Academy		3,000,000,000	-	0%
4	Programu ya Uimarishaji Utowaji Matangazo ZBC		12,337,261,000	-	0%
5	Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa		5,000,000,000	-	0%
6	Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji		2,000,000,000	-	0%
	Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)		**32,737,261,000**	**560,000,000**	**2%**
	JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)		**49,081,861,000**	**12,223,435,806**	**25%**

KIAMBATISHO NAMBA 1B

MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023

MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	260,000,000	164,857,500	63%
2	Baraza la Kiswahili Zanzibar	25,000,000	9,846,509	39%
3	Habari Maelezo	120,000,000	23,038,750	19%
4	Tume ya Utangazaji	300,000,000	142,807,950	48%
5	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	81,000,000	113,520,908	140%
6	Ofisi kuu Pemba	89,997,000	37,937,500	42%
	JUMLA	**875,997,000**	**492,009,117**	**56%**

KIAMBATISHO NAMBA 1C

MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO.	TAASISI	BAJETI 2021/2022	MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2021 HADI MACHI 2022	ASILIMIA
2	Shirika la Utangazaji (ZBC)	1,400,000,000	697,064,761	**50%**
3	Shirika la Magazeti	1,011,900,000	621,226,037	**61%**
4	ZAGPA	4,700,000,000	2,238,643,637	**48%**
5	ZMUX	1,500,000,000	1,188,537,023	**79%**
	JUMLA	**8,611,900,000**	**4,745,471,458**	**55%**

KIAMBATISHO NAMBA 1D

FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Maendeleo ya Vijana	293,899,000	209,660,385	71%
2	Baraza la Vijana Zanzibar	351,900,000	143,375,000	41%
3	Programu ya Ajira kwa Vijana	6,400,000,000	-	0%
	JUMLA	**7,045,799,000**	**353,035,385**	**5%**

Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Utamaduni na Sanaa	2,173,471,000	1,820,756,710	84%
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	244,600,000	103,700,600	42%
3	Baraza la Kiswahili Zanzibar	303,900,000	174,524,000	57%
4	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	635,800,000	344,115,551	54%
5	Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa	5,000,000,000	-	0%
	JUMLA	**8,357,771,000**	**2,443,096,861**	**29%**

Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Michezo	310,000,000	99,000,000	32%
2	Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar	173,200,000	41,624,000	24%
3	Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo pamoja na ujezi wa Academy	7,000,000,000	560,000,000	8%
	JUMLA	**7,483,200,000**	**700,624,000**	**9%**

Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	2,137,000,000	1,515,987,425	71%
	JUMLA	**2,137,000,000**	**1,515,987,425**	**71%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	160,800,000	44,000,000	27%
	JUMLA	**160,800,000**	**44,000,000**	**27%**

Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2022	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Idara ya Habari Maelezo	972,500,000	563,110,245	58%
2	Shirika la Utangazaji ZBC	4,376,800,000	3,035,588,430	69%
3	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	421,000,000	134,508,000	32%
4	Shirika la Magazeti ya Serikali	1,283,700,000	804,701,005	63%
5	Programu ya Uimarishaji Utowaji Matangazo	12,337,261,000	-	0%
	JUMLA	**19,391,261,000**	**4,537,907,680**	**23.4%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Tume ya Utangazaji	384,300,000	469,888,670	122%
3	Wakala ya SMZ wa Uchapaji (ZGP)	1,204,500,000	1,394,530,085	116%
4	Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji	2,000,000,000	-	0%
	JUMLA	**3,588,800,000**	**1,864,418,755**	**52%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI 2022/2023	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Ofisi Kuu Pemba	917,230,000	764,365,700	83%
	JUMLA	**917,230,000**	**764,365,700**	**83%**

KIAMBATISHO NAMBA 1E

FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	260,000,000	164,857,500	63%
2	Baraza la Kiswahili Zanzibar	25,000,000	9,846,509	39%
3	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	81,000,000	113,520,908	140%
	JUMLA	**366,000,000**	**288,224,917**	**79%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Habari Maelezo	120,000,000	23,038,750	19%
3	Shirika la Magazeti	1,011,900,000	621,226,037	61%
4	Shirika la Utangazaji (ZBC)	1,400,000,000	697,064,761	50%
6	Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX)	1,500,000,000	1,188,537,023	79%
	JUMLA	**4,031,900,000**	**2,529,866,571**	**63%**

Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Tume ya Utangazaji	300,000,000	142,807,950	48%
2	Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP)	4,700,000,000	2,238,643,637	48%
	JUMLA	**5,000,000,000**	**2,381,451,587**	**48%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023	ASILIMIA
1	Ofisi Kuu Pemba	89,997,000	37,937,500	42%
	JUMLA	**89,997,000**	**37,937,500**	**42%**

KIAMBATISHO NAMBA 1F
BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNINA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024
TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

No	IDARA	MAELEZO	BAJETI 2023/2024
1	Afisi Kuu Pemba	Mishahara	888,192,000
		Matumizi Mengineo	261,800,000
JUMLA			**1,149,992,000**
2	Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	168,000,000
JUMLA			**168,000,000**
3	Uendeshaji na utumishi	Mishahara	1,432,680,000
		Matumizi Mengineo	792,254,000
JUMLA			**2,224,934,000**
4	Habari Maelezo	Mishahara	698,064,000
		Matumizi Mengineyo	200,200,000
JUMLA			**898,264,000**
5	Maendeleo ya Vijana	Mishahara	215,268,000
		Matumizi Mengineo	167,030,000
JUMLA			**382,298,000**
6	Utamaduni na Sanaa	Mishahara	2,220,996,000
		Matumizi Mengineo	276,500,000
JUMLA			**2,497,496,000**
7	Michezo	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	300,300,000
JUMLA			**300,300,000**
Jumla ya Mishahara			**5,455,200,000**
Jumla ya Matumizi mengine			**2,166,084,000**
Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku			**7,621,284,000**

TAASISI ZA RUZUKU

1	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	1,118,297,000
		Matumizi Mengineo	-
			1,118,297,000
2	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	3,394,500,000
		Matumizi Mengineo	1,543,000,000
			4,937,500,000
3	Wakala wa Serikali wa Uchapaji	Mishahara	1,834,300,000
		Matumizi Mengineo	-
			1,834,300,000
4	Tume ya Utangazaji	Mishahara	414,800,000
		Matumizi Mengineo	114,500,000
			529,300,000
5	Kampuni ya Unganishaji Maudhui (ZMUX)	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	294,650,000
			294,650,000
6	Baraza la Vijana	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	246,300,000
	JUMLA		**246,300,000**
7	Afisi ya Msajili Hakimiliki	Mishahara	273,000,000
		Matumizi Mengineo	302,100,000
	JUMLA		**575,100,000**
8	Baraza la Kiswahili Zanzibar	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	212,700,000
	JUMLA		**212,700,000**
9	Baraza la Sanaa,Sensa ya filamu na Utamaduni	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	171,200,000
	JUMLA		**171,200,000**
10	Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	121,300,000

		Matumizi Mengineo	212,700,000
	JUMLA		**212,700,000**
9	Baraza la Sanaa,Sensa ya filamu na Utamaduni	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	171,200,000
	JUMLA		**171,200,000**
10	Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar	Mishahara	-
		Matumizi Mengineo	121,300,000
	JUMLA		**121,300,000**
	Jumla ya Mishahara Ruzuku		**7,034,897,000**
	Jumla ya matumizi mengineo ruzuku		**3,005,750,000**
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**10,040,647,000**
	Jumla ya Mishahara kwa Wizara		**5,455,200,000**
	Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara		**2,166,084,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A		**17,661,930,000**

	MIRADI YA MAENDELEO	
	Ujenzi na Uimarishaji wa viwanja vya Michezo vya Wilaya.	12,000,000,000
	Uimarishaji wa viwanja vya Michezo	21,000,000,000
	Ujenzi wa Viwanja vya Michezo	1,278,054,000
	Jumla ya Miradi ya Maendeleo B	**34,278,054,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (A + B)	**51,939,984,000**

KIAMBATISHO NAMBA 1G

BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Idara ya Maendeleo Vijana	382,298,000
2	Baraza la Vijana Zanzibar	246,300,000
	JUMLA	**628,598,000**

Programu Ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Idara ya Utamaduni na Sanaa na Michezo	2,497,496,000
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	171,200,000
3	Baraza la Kiswahili Zanzibar	212,700,000
4	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	575,100,000
	JUMLA	**3,456,496,000**

Programu Ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Idara ya Michezo	300,300,000
2	Baraza la Michezo	121,300,000
3	Mradi wa ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo	34,278,054 ,000
	JUMLA	**34,699,654,000**

Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	168,000,000

Programu Ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	2,224,934,000
	JUMLA	**2,224,934,000**

Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
1	Tume ya Utangazaji	529,300,000
2	Idara ya Habari Maelezo	17,700,000
3	Wakala wa Serikali wa Uchapaji	1,834,300,000
	JUMLA	**2,381,300,000**

Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024 MATUMIZI
	Ofisi Kuu Pemba	1,149,992,000
	JUMLA	**1,149,992,000**

KIAMBATISHI NAMBA 1H

MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO.	TAASISI	BAJETI 2023/2024
1	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	220,000,000
2	Baraza la Kiswahili Zanzibar	30,000,000
3	Habari Maelezo	140,000,000
4	Tume ya Utangazaji	254,997,000
5	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	150,000,000
	Ofisi Kuu Pemba	81,000,000
	JUMLA	**875,997,000**

KIAMBATANISHO NO 1I
MAPATO YATAKAYO KUSANYWA NA YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO	TAASISI	MAKUSANYO
1	**Shirika la Utangazaji (ZBC)**	**1,400,000,000**
2	**Shirika la Magazeti**	**2,171,000,000**
3	**ZAGPA**	**11,000,000,000**
4	**ZMUX**	**1,500,000,000**
	JUMLA KUU	**16,071,000,000**

KIAMBATANISHO NO. 2A

ORODHA YA VIJANA WALIOPATIWA WA MAFUNZO MBALI MBALI

S/N	Aina ya Mafunzo	W'ke	W'me	Jumla	Taasisi
1	Mafunzo ya Afya ya Uzazi	19,201	12,020	31,221	Idara ya Maendeleo ya Vijana, YFS, Engender, SDHO, Baba Bora, Zapha+,
2	Mafunzo ya Uongozi na Uzalendo	9,786	8,578	18,364	Idara ya Maendeleo ya Vijana, Zanchange Makers, TAMWA, PYI, SCAUTI, JUVIEKA, CYD, JUVIEKA
3	Ujasiriamali	3,553	6,456	10,009	Idara ya Maendeleo ya Vijana, ZMBF, MYDO, TAYI, YUNA,PDS, YCI, PDS
4	Stadi za maisha	34,479	32,511	66,990	Idara ya Maendeleo ya Vijana, MYO, PDS, SAZANI TRUST, YUNA, ZYF,ZAYOVIO, ZAYDO, ZAYADESA, ZAIADA, PIRO,
5	Ushirikishwaji	1,955	2,015	3,970	Idara ya Maendeleo ya Vijana, CYD, Zanchange Maker,SCAUTI, JUVIEKA, ZAHLIFE,
	Jumla kuu	**68,974**	**61,580**	**130,554**	

ORODHA YA VIJANA WALIOPATIWA MAFUNZO MBALI MBALI KWA UPANDE WA PEMBA

		Wanawake	Wanaume	Total	Taasisi
1	Afya ya Uzazi	16,167	14,345	30,512	UMATI, ZAPHA+,YFS, ZAYCO, WACDES
2	Uzalendo na Uongozi	7,356	6,534	13,890	SCAUTI, PIRO, CYD, ACTION AIDS. SOS,PEMBA COMMUNITY FOREST, NGENARECO, UVIMAWE, ZAYCO, WACDES
3	Ushiriki na Ushirikishwaji	5,319	6,345	11,664	PIRO, CYD, SOS, ACTION AIDS, UVIMAWE, NGENARECO, ZAYCO, WACDES
4	Stadi za Maisha	5,234	4,318	9,552	UMATI, ZAPHA+, ZAYCO, WACDES, PIRO, CYD, UVIMAWE
5	Ujasiriamali	6,127	4,234	10,361	PIRO, CYD, SOS, ACTION AIDS, UVIMAWE, NGENARECO, ZAYCO, WACDES, ACTION AIDS,
	Jumla kuu	**40,203**	**35,776**	**75,979**	

KIAMBATANISHO NO 2B
MCHANGANUO WA VIKUNDI UNGUJA

N	Shughuli	Idadi ya vikundi	W'ke	W'me	Jumla	Idadi ya vikundi vilivyotembelewa 2022/23	Idadi ya vikundi vilivyopata mikopo	Kiwango walichopata	W'ke	W'me	Jumla	Jumla ya Vikundi vipya	Jumla ya vikundi vilivyoomba mikopo
1	Wilaya ya mjini	37	127	119	246	33	3	boti 2 yenye thamani ya milioni 26 kwa kila kimoja, na kikundi kimoja milioni 26	**47**	**58**	**105**	23	32
2	Wilaya ya Magharibi 'A'	43	652	273	925	23	20	184,264,219	400	134	534	-	20
3	Wilaya ya Magharibi 'B'	14	29	42	71	14	2	20,000,000			6	4	9
4	Wilaya ya Kati	55	252	393	645	49	4	gari ya mizigo, milioni 15	37	39	69	7	10
5	Wilaya ya Kusini	21	274	156	430	21	1	Mizinga 15 ya nyuki	11	4	15	7	2
6	Wilaya ya Kaskazini 'A'	16	138	116	254	16	1	5,000,000	15	17	32	6	6
7	Wilaya ya Kaskazini 'B'	7	42	38	80	7	1	1,400,000			25		2
	Jumla	**193**	**1514**	**1137**	**2651**	**163**	**32**	**303,664,219**	**510**	**252**	**786**	**47**	**81**

MCHANGANUO WA VIKUNDI
PEMBA

N	Shughuli	Idadi ya vikundi vyote	W'ke	W'me	Jumla	Idadi ya vikundi vilivyotembelewa 2022/23	Idadi ya vikundi waliopata mikopo	Kiasi walichopata	W'ke	W'me	Jumla	Vikundi vipya	Vilivyoomba mikopo	Waliopata
1	CHAKE CHAKE	64	520	568	1088	23	11	197,500,000	72	83	155	-	27	27
2	MKOANI	97	628	659	1287	32	18	77,400,000	85	134	219	-	30	30
3	WETE	65	623	503	1126	33	4	45,000,000	65	35	100	6	20	20
4	MICHEWENI	43	301	389	690	34	8	46,000,000	53	83	136	-	19	19
		269	**2072**	**2119**	**4191**	**122**	**41**	**365,900,000**				6	96	96

KIAMBATANISHO NAMBARI 3A
VYAMA/VILABU VYA MICHEZO MBALI MBALI VILIVYOSHIRIKI MASHINDANO YA KIMATAIFA 2022/2023

S/N	CHAMA/TIMU	MASHINDANO	MWAKA	PAHALA	MAELEZO
1	Chama cha Mpira wa Wavu (Volleyball) kwa watu wenye Ulemavu wa Akili kwaajili	Mashindano ya Kimataifa (Special Olympic World Games Berlin)	Juni 2023	Berlin-Ujerumani	Timu ipo kwenye maandalizi mazuri ya kushiriki mashindano hayo.
2	Chama cha mpira wa mikono (ZAHA)	Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (ECAF)	Disemba 2022	Zanzibar	Timu ya taifa ya Zanzibar ilipata ushindi wa nne katika mashindano hayo
		Mashindano ya Afrika Mashariki na kati ya IHF Trophy	Oktoba, 2022	Kenya	Timu ya Zanzibar haikuweza kufanya vizuri
3	Chama cha mchezo wa Kabaddi	Mashindano ya Afrika Mashariki	Disemba 2022	Uganda	Timu za Zanzibar wanaume ilipata nafasi ya tatu na timu ya wanawake ilipata ushindi wa nne
4	Chama cha mchezo wa Judo	Mashindano ya klabu bingwa Afrika Mashariki	Disemba 2022	Dar es Salaam	Timu ya Zanzibar ilipata nafasi ya pili na medali 6
		Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati	Aprili 2023	Dar es Salaam	Wawakilishi kutoka Zanzibar walifanikiwa kupata medali 4 (1 Gold, 2 Silver na 1 Bronze) kwa mashindano ya uzito wa Kg 90, kg 81, kg 66 na kg 60.
5	Chama cha mchezo Riadha	Mashindano ya Afrika mashariki na kati ya vijana chini ya umri wa miaka 18 na miaka 20. Mashindano ya kuchaguliwa kushindana mashindano ya kimataifa ya CAA	Machi 2023	Dar es salam	Timu zote mbili kutoka Zanzibar zilipata nafasi ya pili na medali 11 (2 za dhahabu 4 za fedha 5 za shaba). Jumla ya wazanzibari 7 (wanaume na wanawake) wamefanikiwa kufikia vigezo vya kimataifa kwenye mchujo wa Tanzania kushiriki mashindano ya Riadha ya Afrika kwa mita 100, 200, kurusha tufe, kurusha kisahani na kurusha mkuki. Washiriki hawa wataiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo yatakayofanyika Lusaka 27 April hadi 3 Mei 2023

KIAMBATANISHO 3B
VYAMA/VILABU VYA MICHEZO MBALI MBALI VILIVYOSHIRIKI MASHINDANO YA KITAIFA 2022/2023

SNO.	CHAMA	MASHINDANO	PAHALA	MWAKA	MAELEZO
1.	Chama cha Mpira wa Meza	Mashindano ya vilabu	Holi la skuli ya Aden, Shakani	Agosti 2022	Vilabu mbalimbali vya mpira wa Meza vilishiriki katika mashindano hayo.
2.	Chama cha Baskeli	Mashindano ya Taifa	Dar es salaam	Agosti, 2022	Mchezaji mmoja kutoka Zanzibar alipata nafasi ya tatu
3.	Chama cha Netiboli	Mashindano ya Klabu Bingwa ya Tanzania	Morogoro	Oktoba, 2022	Timu ya JKU wanaume ilipata nafasi ya kwanza na KVZ wanawake nafasi ya pili
4.	Shirikisho la Mchezo wa Basketball Zanzibar	Mashindano ya Taifa Cup	Tanga	Oktoba, 2022	Timu ya wanawake kutoka Zanzibar ilipata nafasi ya pili na wanaume walifika katika hatua ya robo finali
5.	Chama cha Baseball and Softball	Mashindano ya Taifa	Dar es salaam	Disemba, 2022	Timu kutoka Zanzibar zilipata nafasi ya pili na ya tatu
6.	Chama cha mchezo wa Judo	Mashindano ya Zanzibar Budokan Cup	Amaan, Zanzibar	Disemba, 2022	Timu mbalimbali kutoka Unguja na Pemba zilishiriki katika mashindano hayo
7.	Chama cha Riadha	Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar	Amaan, Zanzibar	Novemba, 2022	Timu ya KMKM iliibuka kuwa klabu Bingwa ya Zanzibar kwa kupata nafasi ya kwanza
8.	Shirikisho la mchezo wa Nage	Mashindano ya kusherehekea Mapinduzi ya Zanzibar	Zanzibar	Januari, 2023	Timu ya umoja ni nguvu ya Mkokotoni ilipata nafasi ya kwanza na FUFUNI kutoka Mkoani Pemba ilipata nafasi ya pili